

# Majibu ya kuaminika kwa Maswali yako kuhusu Chanjo ya COVID-19

Mei 25, 2021

Chanjo nne za COVID-19 zimeidhinishwa kutumika nchini Canada na mamilioni ya watu wamepokea chanjo hizi ulimwenguni kote. Taarifa hii inashughulikia masuala na maswali ya kawaida juu ya chanjo ili uweze kuwa na taarifa muhimu juu ya kile kinachoingia mwilini mwako unapopata chanjo ya COVID-19. Maelezo katika taarifa hii yamethibitishwa na madaktari na watafiti.



## Je, ninaweza kupatiwa chanjo ikiwa nina mzio?

Ndio, ni salama kwako kupatiwa chanjo ya COVID-19 hata kama una historia ya athari kali za mzio kwa vyakula tofauti, dawa, au vitu vingine. Ikiwa una historia ya athari kali ya mzio, subiri kwenye kituo cha chanjo kwa dakika 30 baada ya chanjo ili kuhakikisha unajisikia VIZURI. Wahudumu wa afya wanapatikana kila wakati kwenye kituo ili kukusaidia iwapo utapata madhara. Ikiwa umepata na mzio mkali kutokana na viungo maalum vya chanjo COVID-19 (kama vile polyethylene glycol [PEG] au polysorbate) au kwa dozi ya kwanza ya chanjo ya COVID-19, unapaswa kuzungumza na mtoa huduma wako wa afya kuhusu jinsi ya kupatiwa chanjo salama. Tafadhalii kumbuka kuwa mzio huu ni NADRA sana.



## Je, ninaweza kupatiwa chanjo ikiwa nina tatizo la kiafya?

Unaweza kupatiwa chanjo salama ikiwa una maradhi kama vile ugonjwa wa kisukari, shinikizo la damu, ugonjwa wa moyo, pumu, au upungufu wa damu.

Iwapo una tatizo **maalum** la kiafya au unatumia dawa ambayo **inadhoofisha mfumo wako wa kinga** (ugonjwa au dawa za kudhoofisha kinga kama vile tibakemikali au tembe za steroidi, nk.) au maradhi ya kingamwili, zungumza na mtoa huduma za afya wako kuhusu siku nzuri kupatiwa chanjo.



## Je, ninapaswa kusubiri hadi watu wengi wapatiwe chanjo?

Hapana. Pata chanjo mara tu zamu yako ikifika. Itakukinga dhidi ya kuugua au kufa kutokana na COVID-19. Kuanzia Mei 25, zaidi ya dozi bilioni 1 za chanjo za COVID-19 zimetolewa kwa watu kote ulimwenguni. Ili kumaliza ugonjwa huo, watu wengi wanapaswa kupokea chanjo; kadri watu wanavyopata chanjo, ndivyo jamii zetu zitakuwa salama.



## Chanjo inanilinda kwa muda gani?

Watafiti bado wanajaribu kubaini chanjo hizo hutoa kinga kwa muda gani. Unaweza kutakiwa kupatiwa dozi za ziada katika siku zijazo kwa ajili ya kinga endelevu ya virusi vya COVID-19.

Chanjo za COVID-19 zinatolewa ama kwa dozi moja au mbili, kutegemeana na chanjo yenye. Ikiwa chanjo unayopokea inatolewa kwa dozi mbili, utaombwa kurudi kwa ajili ya dozi ya pili siku zijazo. Lazima upate dozi ya kwanza na ya pili ya chanjo ili uweze kupata kinga zaidi dhidi ya homa kali au kifo kutokana na COVID-19.

Kumbuka: Unapaswa kuendelea kufuata hatua zote za usalama za COVID-19, kama vile kuvalaa barakoa, kutotangamana na wengine, na kunawa mikono, hata baada ya kupata chanjo.

Chanjo zinakukinga wewe na watu unaowapenda dhidi ya kuugua COVID-19. Kadri watu wanavyopatiwa chanjo, ndivyo kila mtu anakuwa anakingwa!



**Tunatumai taarifa hii itakufaa! Tunakuomba usambaze taarifa hii kwa kiasi kikubwa, uitumie kama hati ya kurekodi faili la sauti au video, au kuitafsiri katika lugha zaidi ili kuisambaza kwa wengine. Tafadhalii hakikisha umetaja chanzo: Women's College Hospital, OCASI, TAIBU Community Health Centre and Refugee 613.**

**Toleo la Mei 25, 2021**

Maelezo yaliyo katika taarifa hii yamethibitishwa na madaktari wa Canada: Meb Rashid MD, Profesa Msaidizi, Chuo Kikuu cha Toronto; Vanessa Redditt, MD, Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Toronto; na Isaac I. Bogoch, MD, Profesa Mshirika, Chuo Kikuu cha Toronto

{REFUGEE}613

BE IN GOOD HEALTH  
**TAIBU**  
COMMUNITY  
HEALTH CENTRE

**OCASI**  
Ontario Council of Agencies Serving Immigrants

**WCHI**  
WOMEN'S COLLEGE HOSPITAL  
Healthcare | REVOLUTIONIZED

Funded by:



Immigration, Refugees and Citizenship Canada

Financé par :

Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

With contributions from:

**pchs**  
Serving Diverse Communities



Occupational Health Clinics for Ontario Workers Inc.

